

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Anuani ya Simu "TAMISEMI" DODOMA
Simu Na: +255 26 2321607
Nukushi: +255 26 2322116
Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz



Mji wa Serikali – Mtumba,
Mtaa wa TAMISEMI,
S.L.P. 1923,
41185 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

**UFAFANUZI KUHUSU VIDEO INAYOSAMBAA IKIONYESHA MIUNDOBINU ISIYO
NA VIWANGO KWENYE UJENZI WA JENGO LA UTAWALA LA HALMASHAURI YA
WILAYA YA SENGEREMA**

Video inayosambaa kwenye mitandao ya kijamii ikionyesha Mbunge wa Jimbo la Sengerema **Mhe. Hamis Tabasamu** akionyesha miundombinu isiyo na viwango kwenye ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema.

Ofisi ya Rais –TAMISEMI inatambua suala hilo na ilishachukua hatua hata kabla ya video hii kusambazwa mitandaoni. Timu mbalimbali za uchunguzi zilishatumwa na kuwasilisha taarifa zake na kufanyiwa kazi.

Mpaka sasa watumishi 3 wa Halmashauri hiyo wameshapelekwa Mahakamani kupitia Taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa (TAKUKURU) kwa tuhuma za matumizi mabaya ya madaraka pamoja na ukiukwaji wa sheria na kanuni za manunuzi ya umma.

Ofisi ya Rais-TAMISEMI inaendelea kuwataka viongozi na watendaji wa Halmashauri zote nchini kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi yote katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kudhibiti ubadhirifu na kuzingatia ubora katika utekelezaji wa miradi hiyo.

A handwritten signature in blue ink, appearing to be 'Nteghenjwa Hosseah'.

Nteghenjwa Hosseah
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Rais –TAMISEMI
27.12.2021